

# **HALMASHAURI YA MANISPAA YA MUSOMA.**

## **SHULE YA SEKONDARI NYAMITWEBIRI.**

### **S.L.P. 1427, MUSOMA.**

**MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI NYAMITWEBIRI KWA MWANAFUNZI KIDATO CHA KWANZA - 2021.**

**JINA LA MWANAFUNZI .....**

#### **1. UTANGULIZI.**

Ninafurahi kukuaarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii mwaka 2021. Unatakiwa kuripoti shulen i kuanzia tarehe **11/01/2021** saa 1 asubuhi, masomo yanayofundishwa ni **Basic Mathematics, Physics, Chemistry, Biology, History, Geography, English Language, Kiswahili na Civics.**

#### **2. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA.**

##### **SARE ZA SHULE**

##### **WAVULANA.**

Suruali rangi ya damu ya mzee 2 (isiwe modo), shati mikono mifupi nyeupe 2, (tetroon), viatu vya ngozi vyeusi vya kamba vyenye kisigino kifupi na visivyo chongoka mbele, soksi nyeusi, tai ndefu (rangi damu ya mzee) na mkanda mweusi wa ngozi. Pia T-shirt zinapatikana shulen.

##### **WASICHANA**

Sketi mbili rangi damu ya mzee zenyelinda boksi mbele na nyuma ndefu inayozidi magoti na yenye pindo lisilozidi inchi mbili, shati mbili nyeupe mikono mifupi, tai damu ya mzee, viatu vya ngozi vyeusi vya kamba vyenye kisigino kifupi visiwe na urembo wowote, soksi nyeupe jozi mbili. Kwa wale wanaovaa hijabu rangi ya hijabu ifanane na sare ya shule. Pia hijabu iwe ndefu usawa wa magoti. Pia T-shirt zinapatikana shulen

##### **NB:**

Haturuhusu viatu laini (vyatya simple), bajaji, modo, na urembo wa aina yoyote. (wote wasichana kwa wavulana). **Pia mwanafunzi mwenye ugonjwa wa kudumu aje na cheti kilichothibitishwa na daktari wa Hospitali teule ya Wilaya au Mkoa.**

#### **3. VIFAA VYA MADARASANI.**

Madaftari makubwa kumi na tano (15 counter books), mathematical set moja, dictionary (English – English au English – Kiswahili Dictionary), four figure moja na kalamu nyeusi au bluu.

#### **4. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE.**

- a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
- b) Mahudhurio mazuri katika shughuli za shule ndani na nje ya shule ni muhimu.
- c) Kuwahi katika shughuli za shule na nyingine utakazopewa
- d) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wa uanafunzi wako katika shule hii.
- e) Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule.
- f) Kuva sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
- g) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.

#### **5. MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA SHULE.**

- a) Wizi
- b) Uasherati na ushoga
- c) Ubakaji
- d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevyta kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli na kadhalika
- e) Kupiga au kupigana
- f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
- g) Kudharau bendera ya Taifa.
- h) Kuoa au kuolewa
- i) Kupata mimba au kusababisha mimba ndani na nje ya shule.
- j) Kutoa mimba
- k) Kugoma au kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
- l) Kukataa adhabu kwa makusudi
- m) Wanafunzi kuwa na simu ya mkononi, kuja na silaha au redio shulenii

**Tafadhali soma kwa makini maelezo au maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.**

Karibuni sana katika shule yetu.

---

**MOJA MWANDU  
MKUU WA SHULE  
0752850815**

# **NYAMITWEBIRI SECONDARY SCHOOL**

## **MEDICAL EXAMINATION FORM**

To be completed by Medical Officer in respect of all form 1 Students.

Full Name .....

Age ..... years. Sex .....

Blood clotting (ESR) .....

Stool examination .....

Urine Analysis.....

Syphilis test.....

T.B Test.....

Chest \_\_\_\_\_

Abdomen \_\_\_\_\_

Pregnancy test \_\_\_\_\_

Additional information of physical defects of impairments (s)

Infections chronic or family diseases

Signature \_\_\_\_\_

Designation\_\_\_\_\_

Station \_\_\_\_\_

Date \_\_\_\_\_